Kukata Mzingo Kwa Mota Iliyoimara

(Cutting Corners With Untempered Morter)

na

Ellis P. Forsman

Kukata Mzingo Kwa Mota Iliyoimara

na

Ellis P. Forsman

Dec 2, 2018

Kukata Kona Kwa Udongo Usioimara

Ezekieli 13:1-15

Wengi wanaacha mwelekeo mzuri uliotolewa kwenye Biblia, na wanakata kona ili kuepuka kufuata maelekezo yaliyotolewa na Mungu. Yesu alitoa mwongozo tunaopaswa kufuata, lakini wengi wanataka kufuata mwongozo wake kwenye barua. Matika Mat. 7:24-27, alisema kama tukimsikiliza na kufuata mwongozo unaotolewa na neno lake tutakuwa wajenzi werevu na nyumba yetu ya kiroho itasimama na kueepuka dharuba ya maisha haya.

"*Basi kila asikiaye hayo maneno yangu na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, alaiyejenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa.*" (Mat. 7:24-27).

Leo Wakristo wengi wanajenga nyumba zao za kiroho na udongo usio imara. Neno "Udongo Usioimara" ipo katika Agano la Kale na inapatikana tu katika kitabu cha Ezekieli. Lynell pamoja na mimi tulikutana na kifungu hiki wakati wa masomo yetu ya kila siku na nikasema kwamba hii inawezaa kuwa somo zuri.

Mungu anamwambia Ezekieli jinsi watu walivyokuwa wanatumia udongo usioimara. "*Kisha neno la BWANA likanijia kusema. Mwanadamu, tabiri juu ya manabii wa Israeli wanaotabiri, uwaambie wanaotabiri* ***kwa mioyo yao wenyewe, lisikieni neno la BWANA; Bwana MUNGU asema hivi; Ole wao manabii wajinga, wanaifuata roho yao wenyewe, wala hawakuona neno lolote!*** *Ee Israeli, manabii wako wamekuwa kama mbweha, mahali palipo ukiwa. Hamkupanda kwenda mahali palipobomolewa , wala hamkuitengenezea nyumba ya Israeli boma, wapate kusimama vitani siku ya BWANA, wameona ubatili na uganga wa uongo, hao wasemao BWANA asema; lakini BWANA hakuwatuma; nao wametumainisha watu ya kuwa neno lile litatimizwa. Je hamkuona maono ya bure, hamkunena mabashiri ya uongo? Nanyi mwasema, BWANA asema, ila mimi sikusema neno. Basi tazzama Bwana*

MUNGU asema hivi; ***kwa sababu mmenena ubatili, na kuona uongo****, basi kwa sababu hiyo, mimi ni juu yenu, asema Bwana MUNGU. Na mkono wangu utakuwa juu ya manabii wanaoona ubatili, na kutabiri uongo; hawatakuwa katika mashauri ya watu wangu, wala hawataandikwa katika maandiko ya nyumba ya Israeli, wala hawataingia katika nchi ya Israeli; nanyi mtajua ya kuwa mimi ndimi Bwana MUNGU. Kwa sababu hiyo, kwa sababu wameshawishi watu wangu wakisema amani; wala hapana amani; na* ***mtu mmoja ajengapo ukuta tazama waipaka chokaa isiyokorogwa vema; basi waambieni hao wanaoupaka ukuta chokaa isiyokorogwa vema, ya kwamba utaanguka****; kutakuwa mvua ya kufurika; nanyi enyi mvua ya mawe ya barafu, mtaanguka na upepo wa dhoruba utaupasua. Na huo ukuta utakapoanguka, je hamtaambiwa, ku wapi kupaka kwenu mlikoupaka? Basi Bwana MUNGU asema hivi; nitaupasua kwa upepo wa dhoruba kwa ghadhabu yangu; tena kutakuwa mvua ya barafu ya kufurika katika hasira yangu; na mawe makubwa katika hasira ya kuukomesha.* ***Ndivyo nitakavyoubomoa ukuta mlioupaka chokaa isiyokorogwa vema, na kuuangusha chini hata misingi yake itafunuliwa; nao utaanguka nanyi mtaangamizwa katikati yake; nanyi mtajua ya kuwa mimi ndimi BWANA. ndivyo nitakavyoitimiza ghadhabu yangu juu ya ukuta ule, na juu ya walioupaka chokaa isiyokorogwa vema; nami nitawaambien, ukuta huo hauko sasa, wala wao walioupaka hawako***." (Ezekieli 13:1-15)

Kuhusu chokaa isiyokorogwa vema.

Chokaa ni kitu cha ajabu. **"KAMA"** kama ikikorogwa vizuri kwa kiwango kizuri, itakaa kwa karne! Wakandarasi wamechukua chokaa ya zamani kutoka kwenye matofari, moshi uliogandamana katika tofari iliyotengenezwa na chokaa na katika hali nyingine sehemu ya nje itavunjika badala ya palipounganishwa na chokaa.

Mkadiriaji mzuri wa chokaa anayeruhusiwa kutibu na kupaka kwenye kiunganishi ikiwa na nguvu kama kifaa kinachounganishwa pamoja. Ili iweze kuwa nzuri hivyo, kila kitu kinapaswa kuwa sawa kama maelekezo yalivyo.

Lazima iwe na idadi kamili ya mchanga, idadi kamili ya chakaa, na kipimo halisi ya maji. Na inapaswa kupakwa kabla haijakauka. Kwa kazi ya serikali, choka ina ukomo wa wake wa kukorogwa kabla haijatumika. Muda ukiisha, humwagwa na nyingine kutengenezwa ili kuhakikisha kwamba nguvu itakuwa kubwa na itakaa kwa muda. Kitu chochote kilichopungufu hukauka kwa muda mfupi sana.

Hiyo pia inaweza kusemwa kwa nguvu zetu za kiroho.

Tunapaswa kufuata maelekezo kwa barua, kukaa sawa, kutunza moyo usiharibike, na kila wakati kukoroga, unaongeza, na kutumia kile tu ambacho Mungu ametupatia.

Umewahi kusikia watu wakisema, "*Makanisa ya Kristo, hufanana, jana leo, na kesho.*" Msemo huu unaweza ukawa na bangili unaofanana. "*Yesu Kristo ni yeye yule jana na leo na hata milele.*" (Heb. 13:8).

Hataivyo, inaonyesha ama ukweli wa maandiko au ukweli wa historia. Makanisa ya Kristo yanafanya hivyo. Maelekezo ya Mungu hayajawahi kubadilika, lakini makanisa katika historia yamebadilika.

Kwa mfano, kanisa la Efeso lilikuwa na mwanzo na mwisho. Katika Matendo ya Mitume 20:29-31, mtume Paulo aliwaonya wazee wa Efeso: "*Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa mwitu wakali wataingia kwenu wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wajisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao. Kwa hiyo kesheni mkikumbuka ya kwamba miaka mitatu usiku na mchana sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi.*" (Mdo. 20:29-31)

Kwanza kanisa la Efeso liliwakataa waalimu wa uongo, na walisifiwa na Bwana kwa hili. Lakini mara, liliacha upendo wake wa kwanza (Ufu. 2:1-4). Isipokuwa wakitubu, Bwana alihaidi angeliondoa (Ms. 5)

Historia inaonyesha kwamba kanisa la Efeso lilitoweka. Tunapoangalia alichokisema Paulo kwa wazee wa Efeso katika Matendo 20: 29-31, tunaweza kuona mwendelezo: baada ya kupoteza upendo na shauku kwa ambaye alikuwa mwema na akawaokoa, wao (kanisa) walionywa katika matakwa yao ya "*…kuishindania imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja.*" (Yuda 1:3).

Kama matokeo, walianza kuruhusu waalimu wa uongo ambao hapo mwanzo walisimama imara na kuwakataa. Ghafla, na viongozi wao wakaanza kufundisha vitu vilivyokuwa vya uongo. Kutumia maelezo ambayo ilitumiwa kabla kuelezea Israeli ya kimwili iliyoanguka walijenga ukuta wa usalama na "*kuupaka ukuta chokaa isiyokorogwa vema*" (Ezekieli 13:10-11)

Leo hii, inaonekana kwamba wengi miongoni mwetu wanajaribu kujenga ukuta wa umoja na kuweka chokaa ya usalama isiyokorogwa vyema sura ya 14 ya Warumi na kuruhusu kila aina ya vitu vibaya kufanyika katika ibada ya kanisa – kwa sababu ya umoja.

Hataivyo, hakuna chochote kibaya kwa umoja wa kweli na usalama tunayopewa katika Kristo, lakini ukuta uliojengwa na mwanadamu ya

umoja wa uongo na usalama unaojengwa na chokaa isiyokorogwa vema inatarajiwa kuanguka chini.

Kama Israeli ya zamani, makanisa mengi yapo kwenye wakati mugumu leo; lakini badala ya kuukubali alafu wafanye kitu juu yake, badala yake wanahimizwa na wale wanaolia, "*Amani wakati hakuna amani*" (Ezekieli 13:10, Yeremia 6:14; 8:11). "Vikombe vingi, ndio! Vyombo vya muziki, ndio! Wakati Mungu hajaviruhusu.

Kilio hiki kinasikiwa leo katika ujumbe wa wale wanao hubiri na kufundisha kwamba mambo siyo mabaya kama yanavyoonekana, na kwamba makanisa ni bora kuliko yalivyokuwa hapo awali.

Katika matukio yote, hii siyo kweli. Hataivyo, Wakristo wengi wamenaswa katika dhana potovu ya usalama.

Kama jinsi ukuta wetu tuliojijengea wa umoja na usalama unavyokuja kutuangukia wale waliokusudia kujenga matakwa yao binafsi kwa wasikilizaji wao kwa kulia "*Amani, amani,' wakati hakuna amani*" wametibu jeraha la "*watu wa* [Mungu] *kidogo*" (Yeremia 6:14). Hawa wahubiri wa kisasa hawajatibu chochote. Kwa ukweli, wameongeza tatizo.

Kwa jina umoja hiyo itatufanya kuwa na usalama katika kupotosha na kugawanya kwa maelefu ya makundi tofauti, kila mmoja na mafundisho yake, ambayo itatufanya kuruhusu kila aina ya mafundisho ya uongo, inatumika kujenga ukuta uliowekwa pamoja na chokaa isiyokorogwa vema.

Ni kweli kwamba mafundisho ya Warumi 14 ilikusudiwa kutunza umoja katika makanisa. Hii inafanywa kwa kuwafundisha Wakristo wasigawanyike katika mambo yasiyo ya msingi, lakini kanuni iliyofundihwa katika Warumi 14 haikukusudiwa kufundisha makanisa kwamba wanapaswa kudharau mafundisho ya uongo, au kumdharau yule anayefundisha. Miongoni mwetu wale wanaojaribu kutumia Warumi 14 kwa njia hii "wamepaka ukuta chokaa isiyokorogwa vema".

Kipimo cha mwisho cha kutokuelewa na kutotumia vyema Warumi 14 haitowi umoja na usalama katika ahadi. Kinyume, kama chokaa isiyokorogwa vyema itasababisha ukuta kuanguka, kuruhusu mafundisho ya uongo hakika inajenga tabia za ajabu miongoni mwa makanisa ya Kristo.

Hitimisho

Mungu ametuonya kuhusu kuwa na hakika kwamba chokaa yetu ya kiroho haikorogwi vibaya, na anatuambia kwamba mwanadamu hajaitim kutengeneza njia yake mwenyewe ya kiroho na kufikiri kwamba kuna njia inayokwenda mbinguni tofauti na ambayo Mungu amesema.

- Yer. 10:23, "*…njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake; ; kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu.*"

- Mit. 16:25, "*iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mt; lakini mwisho wake ni njia ya mauti.*

Kuta za chokaa isiyokorogwa vema itashindwa.

Mungu anatuambia kwamba tunapaswa kujifunza neno lake, tuache njia zetu wenyewe, na kufanya sawasawa na alivyotuagiza.

- Isa. 55:7, "*Mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake; na amrudie BWANA, naye atamrehemu; na arejee kwa Mungu wetu, naye atamsaidia kabisa.*"

- 2 Tim. 2:15-19, "*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli. Jiepushe na maneno yasiyo na maana, ambayo si ya dini; kwa kuwa wataendelea zaidi katika maovu, na neno lao litaenea kama donda ndugu. Miongoni mwa hao wamo Himenayo na Fileto, walioikosa ile kweli, wakisema ya kwamba kiyama imekwisha kuwapo, hata kuipindua imani ya watu kadhaa wa kadhaa. Lakini msingi wa Mungu ulio imara umesimama, wenye muhuri hii Bwana awajua walio wake. Na tena kila alitajaye jina la Bwana na auache uovu.*"

Katika maneno yake yaliyoandikwa ametuambia – ametuonya – kuwa sawa na neno lake na tusifanye badiliko lolote. "*Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lolote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.*" (Ufu. 22:18-19).

Tuhakikishe chokaa yetu inakorogwa vyema na kuweka makanisa yetu kuwa na nguvu na umilele.